# MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI JANUARY, 2023 NA MWELEKEO KWA MWEZI FEBRUARY, 2023.

**Dondoo za tathmini ya January, 2023 na mwelekeo wa Februari, 2023:**

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Januari, 2023 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa kwa mwezi Februari, 2023 nchini.

- Kipindi cha mwezi Januari 2023, maeneo mengi ya nchi yalipata mvua zilizosababishwa na uwepo wa Ukanda Mvua nchini pamoja na kimbunga 'CHENESO' kilichotokea katika eneo la kaskazini mwa kisiwa cha Madagascar na kusababisha ongezeko la mvua katika baadhi ya maeneo nchini hususan katika wiki ya tatu ya mwezi Januari.
- Katika mwezi Februari 2023, vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka. Hata hivyo, mvua za nje ya msimu zinatarajiwa katika baadhi ya maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka.
- Vipindi vya joto vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo ya nchi hususan yale yanayotarajiwa kuwa na upungufu wa mvua.

## 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JANUARI, 2023.

Katika kipindi cha mwezi Januari 2023, maeneo mengi ya nchi yalipata mvua. Aidha, kutokea kwa kimbunga 'CHENESO' katika eneo la kaskazini mwa kisiwa cha Madagascar kulisababisha vipindi vya mvua kubwa katika baadhi ya maeneo ikiwemo, nyanda za kusini magharibi, kanda ya Kati, mkoa wa Ruvuma pamoja na ukanda wa Pwani. Kiwango cha juu cha mvua cha milimita 95.8 kilipimwa katika kituo cha hali ya hewa kilichopo Mahenge mnamo tarehe 16 Januari, 2023 ikifuatiwa na milimita 76.6 na

milimita 74.1 kilichopimwa katika kituo cha hali ya hewa cha kilimo Ilonga (Morogoro) na Songwe mnamo tarehe 18 na 19 Januari, 2023 mtawalia. Vituo vingine vilivyopima mvua zaidi ya milimita 50 kwa siku ni pamoja na kituo cha hali ya hewa Mpanda milimita 54.3 mnamo tarehe 06 Januari, Mahenge milimita 61.9 tarehe 07 Januari na Singida milimita 68.2 mnamo tarehe 12 Januari, 2023.

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI FEBRUARI, 2023

### 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Hali ya joto la bahari katika eneo la kati la kitropiki ya bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuendelea kuwa chini kidogo ya wastani katika kipindi cha mwezi Februari, 2023. Joto la bahari la wastani linatarajiwa katika eneo la magharibi na mashariki mwa Bahari ya Hindi. Hali hii inatarajiwa kusababisha upungufu wa upepo wenye unyevunyevu unaovuma kuelekea maeneo ya pwani. Aidha, katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki karibu na pwani ya Angola, hali ya joto la chini kidogo ya wastani inatarajiwa. Hali hii inatarajiwa kusababisha uwepo wa upepo wenye unyevunyevu kuvuma kuelekea maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na magharibi mwa nchi. Hata hivyo, katika kipindi cha mwezi Februari 2023, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini inatarajiwa kudhoofika kidogo na hivyo kusababisha Ukandamvua kuendelea kubaki kusini mwa nchi.

### 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI FEBRUARI, 2023

Kwa ujumla vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika baadhi ya maeneo ya nchi. Kwa upande mwingine, vipindi vya joto vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo nchini hususan yanayotarajiwa kuwa na upungufu wa mvua. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Februari, 2023. Aidha, upungufu wa mvua unatarajiwa katika wiki ya nne ya mwezi.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika wiki ya kwanza ya mwezi Februari, 2023 ikifuatiwa na upungufu katika kipindi kilichosalia.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache kwa mwezi Februari, 2023.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo katika mwezi Februari, 2023.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo katika kipindi cha mwezi Februari, 2023.

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo. Aidha, upungufu kidogo wa mvua unatarajiwa katika wiki ya tatu ya mwezi Februari, 2023.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Februari, 2023. Aidha, upungufu wa mvua unatarajiwa katika wiki ya tatu ya mwezi.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo kwa mwezi wa February, 2023. Aidha, Upungufu wa mvua unatarajiwa katika wiki ya tatu ya mwezi Februari, 2023.

## 2.3 MATARAJIO KWA MWEZI MACHI, 2023.

Katika kipindi cha mwezi Machi, 2023, mvua zinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo nchini. Kwa upande mwingine, hali ya joto inatarajiwa kuwa ya kawaida katika maeneo mengi ya nchi.

## 2.4 USHAURI

Mvua za Msimu zinaendelea katika baadhi ya maeneo nchini. Aidha, vipindi vya mvua kubwa vinatarajiwa kujitokeza hivyo wananchi wanaoishi katika maeneo yanayoathiriwa na mafuriko wanashauriwa kuendelea kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari zitakazojitokeza.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

Imetolewa tarehe 01 Februari, 2023 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz